# *KUTOKUAMINI HAKUMZUII MUNGU*

Asante sana, Ndugu. Bwana akubariki.

2 Mwajua, imeandikwa katika Neno, “Nilifurahi walipotwambia, ‘Twendeni nyumbani mwa Bwana.’” Um-hum. Mnaona. Mahali hapa pa kupendeza, mazingira ya kupendeza, mchungaji wa kupendeza, na kwaya yake, kanisa zuri sana, sioni ni kwa nini, kukosekane chochote asubuhi ya leo kwa yote tunayohitaji.

3 Hakika ninauthamini wimbo huo, *Mungu Anatosha*. Huo si ni mzuri? Waliimba vizuri sana na—na sauti zao zilizowekwa wakfu, napenda hilo. Ninapenda kitu ambacho ni halisi, ambacho hakina chochote, mwajua, cha kuigiza. Huna-... Ninapenda uimbaji mzuri, lakini si—siwezi kuvumilia sauti iliyofunzwa kupita kiasi, mwajua, mwajua, mimi...kuishikilia mpaka wanakuwa samawati usoni na, mwajua, na kugogomoa kwa namna fulani, ama kuimba kama ndege, ama kitu fulani, na—na, huko si kuimba. Na—napenda kuimba kwa namna hiyo, halisi tu, moja kwa moja kutoka moyoni, uimbaji mzuri wa mtindo wa kale wa Kipentekoste.

4 Ndugu Fred Sothmann, uko hapa mahali fulani? Mmoja wa wadhamini wangu. Angalia kote mahali hapa, hivi ndivyo ningetaka kanisa letu lijengwe nyumbani, pamoja na vyumba hivi vyote vya shule ya Jumapili na kadhalika hapa nyuma namna hiyo. Ninapenda hi—hilo...Niliona hilo muda mfupi uliopita nikija huku. Tuko katika, mchakato wa kujenga kanisa jipya, nami na—napenda hili, napenda hivyo viti, mazulia jinsi yalivyopangwa, ni mazuri. Wala sisemi hivyo kwa kusifia sana jinsi nilivyo, ninasema tu ukweli. Na—napenda hilo, ninaninii tu, ninalipenda.

5 Nafikiri hapa ndipo nilipopaswa kuwa kwanza, nimechelewa tu kwa yapata siku kumi; huyo ni mimi, kwa kawaida huchelewa. Na, lakini mambo mawili ambayo nimejifunza asubuhi ya leo, kwamba hili likiwa ni, moja ya Churches of God kutoka Cleveland, Tennessee. Watu hao wamekuwa baraka kwangu kote ulimwenguni.

6 Ninakumbuka tukio moja tulilokuwa nalo na... tulipofahamiana kwa mara ya kwanza, hapa miaka kadhaa iliyopita, Ndugu Gordon Lindsay, ambaye anashirikiana na Assemblies of God, alinipeleka huko Chattanooga, naye akasema watakuwa na mkutano kule nao walikuwa na ukumbi mkubwa wa mikutano.

7 Kwa hiyo nikamtuma Ndugu Baxter, ambaye alikuwa akinena kwa niaba yangu wakati huo, huko Chattanooga, naye akanipigia simu tena, akasema, "Ndugu Branham, tuna jumba la mikutano hapa, linaloketi watu elfu sita mia tano, tuna kanisa moja linaloudhamini, na ni kanisa dogo kwenye orofa ya chini, katika orofa ya chini, labda tu wafuasi wapatao thelathini na watano." Kasema, "Ni . . . hilo ni zuri," lakini kasema, "hilo ndilo pekee linaloudhamini."

8 Nami nikasema, "Vema, nitakuja huko kesho," nami nikaingia kwa ndege. Basi kesho yake asubuhi nikapata majaliwa ya kuzungumza kwenye Chuo cha Lee, hicho ni kimoja cha vyuo vikubwa, na, loo, hilo lilikuwa ni kundi zuri jinsi gani la wanafunzi. Ndipo kesho yake usiku walipoingia walikuwa wamesongamana huko barabarani, hata wasingeweza kupata nafasi ya kuketi chini mahali popote. Kweli walikuja kuniokoa wakati huo, jumba hilo lote la mikutano, huku kanisa moja dogo sana likiidhamini, nao wote wakakusanyika pamoja, na kweli tulikuwa na wakati mzuri sana.

9 Na hayo yalikuwa ndiyo mawasiliano yangu ya kwanza ya moja kwa moja na makao makuu ya Church of God. Ninapenda jina hilo, The Church of God. Na—napenda jina kama hilo, nami ninawathamini sana.

10 Mnajua, nadhani, Ndugu David Littlefield. Naye ni rafiki msiri wangu sana, yeye huja nyumbani kwangu wakati wote, tunakuwa na ushirika sisi kwa sisi kule juu. Naye ndio kwanza ajenge kanisa jipya nami nilikuwa na majaliwa ya kuliweka wakfu kwa Bwana, hivi majuzi.

11 Na kwa hiyo, tuna furaha kuwa hapa leo, katika mazingira haya mazuri ya ibada. Nami ninathamini sana ma—mahudhurio ya makanisa haya tangu tumekuwa humu mjini, na kote katika hili Bonde la Maricopa, ushirika mzuri sana.

12 Nilisema hivi majuzi ya kwamba nafikiri neno *phoenix* linamaanisha, "kitu ambacho kimetoka pasipo na kitu." Sasa, huenda hilo likawa ni tamshi baya, lakini nafikiri hilo ni jambo la namna hiyo, ya kwamba mji huu ulijengwa kutoka kwenye ja—jangwa hapa, moja kwa moja tu katikati ya jangwa, kwa hiyo umeinuka kutoka katika mchafuko.

13 Basi miaka michache iliyopita niliingia humu mjini, miaka kumi ama kumi na mitano iliyopita, nayo makanisa yalikuwa kidogo yanapigana. Ilikuwa vigumu kupata . . . Walisema, "Vema, kama kundi *hili* litafanya ushirikiano, sisi tuko nje." Mnaona? Na kwa hiyo . . . Lakini sasa ninaona ya kwamba kuna *phoenix* mwingine umeinuka, udugu mzuri sana wa ushirikiano miongoni mwa ndugu, makanisa yote pamoja. Nimeona usiku baada ya usiku mahali pengi, jinsi ninii . . .

14 Sasa, kwa namna fulani inamwangukia sana ndugu yetu wa thamani hapa, kwa sababu hii ni Jumapili asubuhi kuwa hapa.

Na—nami. . .daima tumesema kila mtu anapaswa kuwa kwenye wajibu wake Jumapili asubuhi. Nafikiri wakati wowote mkiwa na ibada, kanisa lenu wenyewe linapaswa kuwa ninii yako, hilo ndilo wajibu wa—wako, hapo ndipo mahali pako ambapo unapaswa kukaa, nami daima nimewazia hilo.

15 Katika miamsho yangu kwa kawaida mimi huifunga ninii. . .Jumapili alasiri, ili kwamba, Jumapili ni ibada ya alasiri, kusudi isitatize makanisa ya Jumapili, na kisha kuwatuma wajumbe wote kutoka kote nchini katika makanisa mbalimbali kushirikiana. Huo ni ushirika wa pamoja, ninaupenda huo.

16 Na sasa, leo hii, kuwa hapa, na kufurahia wakati huu wa ushirika, kabla tu ya kwenda kumalizia sehemu yangu ya mwisho, nijuavyo mimi, kwenye ibada ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Nasi tunatumaini, tukiamini, ya kwamba Mungu atakutana nasi alasiri ya leo kule, na kutusaidia kuleta kitu ambacho kitakuwa *cha faida*, maana miongoni mwa watu hao kuna Waespiskopolia, Wakatoliki, Walutheri, na kadhalika. Nasi tunatumaini ya kwamba labda Mungu atashuka tu katika, njia fulani ambayo ita—ambayo itawaingiza wengi.

Ningetaka kusema jambo hili sasa hivi, sijawahi kujisikia niko nyumbani zaidi maishani mwangu, kwa hiyo, nikisimama tu hapa, kwa hiyo. . .

17 Mmeona katika ushirika wa ndugu wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, kwamba wa—wanaingiza, inaonekana, kama ulimwengu wa ekumeni, Waepiskopalia, Wapresbiteri, mnaiona hiyo—hiyo njaa? Nalo Church of Christ, mamia yao walikutana jana usiku huko Dallas kutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, wale ambao wamenipiga vita kote nchini juu ya uponyaji wa Kiungu, nanyi ndugu. Wakati. . .Na sasa mnaona, ninaamini hata hivyo, kwa kuwa wameanza kuona ushirika wetu, muungano wetu, na Mungu pamoja nasi, hakuna kitu wanachoweza kusema dhidi yake, maana inatendeka tu, hivyo tu. Nami nafikiri hilo ni zuri sana.

18 Lakini sasa kwa Kanisa la Mungu aliye hai, wale wote walio katika Kristo, ningependa kutoa tamshi hili dogo: Je, mliitambua ile saa? Kuna watu wengi sana, unapoingia miongoni mwa watu tu kama hao, na watu ambao, kutoka kwenye makanisa mbalimbali, wao si wa kiroho vya kutosha kupata upambanuzi wake. Mnaona? Hawaupati, wanapenda kucheka, na kumsifu Bwana, na kupiga makelele katika furaha ya Bwana, hilo ni sawa, bali kushuka chini na kuona mahali hilo linakotoka, mnaona, kushuka chini na kutambua kile hilo linamaanisha! Kila kitu kimewekwa katika utaratibu katika Mungu, Yeye yuko kwenye wakati ufaao hasa.

19 Wakati mmoja nilikuwa nikihubiri juu ya somo la *Amri Ya Kumi Na Mo-*. . ., ama, *Ile—Ile Heri Iliyosahaulika*, ndiyo

iliyokuwa. Katika mlango wa 11 wa Mathayo, kifungu cha 6, ilisema ya kwamba Yohana aliwatuma wanafunzi wake huko kutafuta kujua, kumwuliza Yesu kweli Yeye alikuwa ndiye Masihi ama siye. Naye Yesu kamwe hakumpa Yohana kitabu juu ya jinsi ya kuenenda kani-. . ., ama, jinsi ya kutenda gerezani, ama—ama kadhalika, Yeye alisema tu, "Kaeni mpaka ibada iishe, ndipo basi, ndipo mtakapojiamulia wenyewe." Mnaona?

20 Kwa hiyo mambo yakatukia, kwa hiyo wakavuka kilima wakarudi kama walivyofanya, Naye akaanza kusema, "Mlitoka kwenda kumwona nani? Mlitoka kwenda kuona nini? Mtu aliyevikwa mavazi mororo?" Kasema, "Hao wako, majumba ya mfalme. Mlitoka kwenda kumwona nabii?" Kasema, "Zaidi ya nabii." Ndipo akaanza ku—kumsifu Yohana, baada ya Yohana kumpa niniii, kitu duni sana alichoweza, karibu kitu kibaya kuliko vyote alichoweza, alichosema kumhusu Yesu kilikuwa ni kumhoji baada ya yeye kumtambulisha. Ndipo basi Yesu, akigeuka moja kwa moja, na kujua ya kwamba Yohana alikuwa roho ya Eliya hasa . . .

21 Wote wawili walienda wakikemea vikali walivyoweza, na—na kukata, na kuacha vibanzi vianguke vitakapo. Halafu je, mliona? Mara baada ya huduma ya Eliya pamoja na huyo Yezebeli, na watu wote wakijaribu kumwiga yeye na kadhalika (Jinsi hapana shaka alihubiri vikali na kuikatakata Injili hiyo mle ndani siku hiyo!), ndipo hatimaye baada ya kumthibitisha Mungu, kwamba, alikuwa ni Mungu, Mungu alishuka na kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, ndipo akashikwa na fadhaa. Akatoka nje, akaketi chini ya mretemu, naye akataka kufa, na—na akaomba Mungu ayachukue maisha yake, na siku arobaini mchana na usiku alikuwa huko nje nyikani akizungukazunguka, ndipo Mungu akamkuta amejificha katika pango mahali fulani.

22 Je, mliona Yohana akija vivyo hivyo? Mliona jinsi alivyokuja? Vivyo hivyo tu, akikatakata, na kufyeka, na—na kusema, "Si halali kwako kumchukua mke wa ndugu yako," na—na hiyo hatimaye ilimfanya akatwe kichwa chake. Ndipo walipomtupa gerezani, mara tu alipokwisha kumthibitisha Mungu na kumtambulisha, na kusema, "Huyu ndiye Masihi."

23 Ninaamini, katika *Nyakati za Mwanzoni* cha Pember, ama mmoja wa waandishi mashuhuri, alisema ya kwamba Yohana . . . Manabii wote ni tai, bila shaka, inawabidi kupaa juu wapate kuona mbali. Naye alisema jicho lake la tai liliingia utando kwenye gereza hilo. Lakini jambo ni kwamba, yeye alikuwa mfano wa Eliya hasa, mnaona, ilibidi awe na hali hiyo ya kutikiswa.

24 Ndipo tunaona siku hizi. Je, mnatambua ya kwamba miaka hii yote ambayo tumepigania huduma hii, ubatizo huu wa Roho Mtakatifu, baraka za Kipentekoste na kadhalika . . . Inasikitisha

tunapoliangalia kanisa letu na kuona kwamba wengi wao wana—wanarudi nyuma. Lakini, hata hivyo, katikati ya hayo, tunaangalia huku nje na tunafanya macho yetu. . .

25 Wazia kuhusu ulimwengu wa ekumeni ukiingia, Wapresbiteri na Walutheri, lakini geuza hilo sasa, kama una upambanuzi wa kiroho na uangalie ile saa, inaonyesha tumewasili, saa ile ile ambayo yule mwanamwali aliyelala alipokuja kutafuta Mafuta na akaenda kuyanunua, hapo ndipo Bwana-arusi alipokuja. Mnaona, mnaona, mnaona, mnaona?

26 Mnapowaona Wamethodisti, na Wabaptisti, na Presbiteri, na kadhalika, wakitafuta Roho Mtakatifu, iweni waangalifu, hiyo ndiyo ile saa. Wakati mwanawali aliyelala alipoanza kuja, nao wakasema, "Tupeni Mafuta yenu":

Kasema, "Sasa, ninyi nendeni mkayapate kwa njia ile ile, mahali tulipoyapata."

27 Nao walipoenda kuyatafuta, ilikuwa ni saa iyo hiyo ambapo Bwana-arusi alikuja naye Bibi-arusi akaingizwa ndani, nao wakaachwa nje, ambako kulikuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno. Sijui kama watu wangu wa Kipentekoste wamefungua macho yao kwa kitu kama hicho, kutambua tuko moja kwa moja u—ukingoni mwa kuonekana Kwake, wakati wowote tu, hakuna kitu kingine kilichosalia.

28 Ndio kwanza tuzipitie zile *Nyakati Saba Za Kanisa* nyumbani, na mambo hayo yote, na chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu tukiona kila wakati, na jinsi ulivyojigawa wenyewe, na kuingia katika Wakati huu wa Kanisa la Laodikia, na kumwona Kristo akitolewa nje ya kanisa Lake Mwenyewe na kusimama mlangoni akibisha, akijaribu kurudi katika kanisa Lake Mwenyewe, na kuona Ujumbe hasa, na kile kingetokea katika siku hiyo, na jinsi ambavyo yule mwanamwali aliyelala angetenda, na mambo haya yote na yale, na kuliona, kila kitu kikiwa tayari kabisa, sasa hivi, kwamba tu Kunyakuliwa kunaweza kuja wakati wowote, hiyo ni kweli. Nina furaha sana. "Wote wanaopenda kuonekana Kwake!"

29 Mtu fulani alisema hivi majuzi, kasema, "Ndugu Branham, unawatisha watu."

Nikasema, "Unamaanisha nini?"

Kasema, "Vema, ukisema ya kwamba huenda Yesu akaja wakati wowote."

Nikasema, "Wewe ni Mkristo?"

"Naam, lakini, jamani, kuna kazi nyingi ya kufanywa."

30 Nikasema, "Hebu kidogo," nikasema, "tukio kuu sana ambalo lingeweza kutukia, linalouchangamsha moyo wangu kuliko kitu kingine chochote, kujua kuonekana kwa Yesu Kristo." Hiyo ni kweli. Mbona, huu unaopatikana na mauti utachukua kutopatikana na mauti, uzee utaondoka kwake.

Ni—nitaninii . . . Mbona, tuta—tutafanywa katika sura ya Mwana wa Mungu, nasi tutamwona jinsi alivyo, na kupitia . . . Hakutakuwako na kipindi cha wakati tena.

31 Na Umilele! Mbona, nini . . . ? Jamani, mtu ambaye hakupenda kuonekana Kwake angekuwa ana shida ya akili, hiyo ni kusema, kama wewe uko sawa, kama ninii yako—kama nafsi yako iko sawa, ina shauku.

32 Ungeweza kuwazia mwanamume akiwa mbali na mkewe kwa miaka mingi, mke mzuri, mpendwa huku akijua wakati wowote kwamba atajitokeza naye atamwona? Na loo, mbona, matarajio yake yote yanatumainia kumwona mara moja, mnaona, akimtarajia tu kutokea wakati wowote.

33 Ama msichana, mpenzi wake amekuwa hayuko, wanajiandaa kufunga ndoa. Mara tu atakapowasili, watafunga ndoa. Mbona, loo, jamani, jinsi ameweka kila kitu tayari! Jamani, na hiyo . . . Mbona, hakuna kitu duniani cha maana kwake ila tu mvulana huyo kutokea, hivyo tu. Vema, hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa. Naam. Tunapaswa tu kupenda kuonekana Kwake. Kweli . . .

34 Paulo alisema, "Nimewekewa taji, ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa Siku ile," si yeye tu, "bali wote *wanaopenda* kuonekana Kwake." Na—napenda hilo vizuri sana.

35 Vema, angalieni hapa, mimi, jambo pekee, mimi ni *mwenda pole* sana kuanza halafu *muda mrefu* sana kumalizia, na nina furaha sana kwamba ninyi nyote mnaamini katika neema, nanyi—nanyi mnanivumilia. Sasa, hatutachukua ila muda mfupi tu, na kuninii . . . hapa pamoja na kanisa.

36 Na la—laiti kama haingalikuwa tu ni kwa sababu ya kuzungumza nanyi na ahadi niliyokuwa nayo, ningependa tu kusikia maskini kwaya hii ikiimba muda wote uliosalia, na—na ninii—na kanisa huko nje linashuhudia juu ya utukufu wa Mungu, na kile ambacho kimekuwa kikitendeka miongoni mwenu. Loo, hilo lingekuwa ni jambo zuri sana. Ninge—ningelitatua tu papo hapo kwa ajili ya hilo, kuona hilo likitukia.

37 Unajua, sisi wahudumu mara nyingi, ama hasa wainjilisti, daima tunaenda kanisani na inatubidi tu kuendelea kuhubiri, kuhubiri, kuhubiri, kamwe hatuketi chini na kuota moto karibu na ule Moto kanisani, mwajua, kujenga tu ninii . . . mwajua, na . . .

38 Kama wanavyodai ya kwamba Pentekoste sasa ni kitu fulani, wengi wa watu wanasema ilikuwa ni kitu *kilichokuwako*, na miaka mingi sana iliyopita, miaka elfu mbili iliyopita, walikuwa na Pentekoste, naye Roho Mtakatifu akawashukia watu, na—nao wakafanya mambo makuu. Vema sasa, huwezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa. La, utaganda hata kufa. Unaona? Hicho ni kitu tu kilichochorwa kwa rangi, hicho ni kitu *kilichokuwako*.

Na iwapo Mungu aliyekuwa pamoja nao wakati huo si Yeye yule leo, basi . . .

39 Ni kama tu kumlisha kurumbizi wako vitamini apate mbawa nzuri, zenye nguvu, na mifupa mizuri, na manyoya mengi, kisha unamweka kizimbani. Haifai kitu sana kumpa manyoya mazuri ya mbawa kama hutamruhusu aruke kidogo. Kwa hiyo nafikiri hivyo ndivyo inavyotupasa kufikia tu mahali ambapo tunamruhusu Roho Mtakatifu aingie na kutenda kazi miongoni mwetu na kutufanyia jambo fulani.

40 Sasa, tutasoma kwa muda kidogo tu, Maandiko, na kuzungumza nanyi tu kwa dakika chache. Halafu basi yapata saa nane. . .Inawabidi kwenda nyumbani na kula chakula cha kutwa, kisha mrudi, na saa nane ninapaswa kuwa tena kwenye mkutano wa Wafanyabiashara kuhubiri alasiri ya leo.

41 Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu, kabla hatujaomba. Nami nashangaa asubuhi ya leo, katika uchaji wa majira haya, kwamba ikiwa mioyoni mwetu tuna mzigo ambao tungetaka Mungu ajue habari zake, nawe ungetaka kukumbukwa katika maombi, kama ukiinua tu mkono wako. Bwana awabariki.

42 Mungu Mwenyezi na Mweza yote, Yeye Asiye na Kikomo, Aliyekuwako, kabla hapajakuwapo na ulimwengu, atomi, ama molekuli, aliketi pale katika Umilele, yule MIMI NIKO aliye mkuu. Jinsi tunavyokushukuru Wewe leo kwamba Wewe umetufanyia njia ya kuja Kwako na—na kuweza kufanya mahojiano na Wewe, kwa maana ilisemwa na Mwa—Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, Mwokozi wetu, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya."

43 Basi tunaomba katika Jina la Yesu mazungumzo mafupi tu pamoja Nawe, Bwana, kwa sababu tunakupenda, nasi tunataka kujieleza Kwako. Tunakupenda kwa sababu Wewe ulitupenda, wala tusingekuwa hapa isingalikuwa ni Wewe. Ndipo tulipokuja kwa njia ambayo tulifika hapa, ndipo Yesu alikuja kutukomboa kurudi kwa huyu Baba mwenye upendo.

44 Nasi tungeomba asubuhi ya leo kwamba katika nuru ya nguvu za kutakasa za Damu Yake kwamba ungetusafisha na uovu wetu wote, lolote ambalo tumefanya, kuwazia, ama kusema ambalo lilikuwa kinyume na Wewe, na Baba Mungu, tunajua ya kwamba hayo yangekuwa ni mambo mengi. Kwa kuwa Mungu mkuu Mtakatifu hata Malaika wanaonekana wachafu Kwake, tungesimama wapi sisi?

45 Lakini leo hii tuna majaliwa ya kuja mbele zaidi ya Malaika, kwa sababu Yesu kamwe hakufa kwa ajili ya Malaika. Na Malaika ni watumishi, na kwa Damu ya Yesu sisi ni wana na binti. Nasi tunakuja Mbele Zako kusema, "Asante, Baba, kwa yale uliyotufanyia, yale unayomaanisha kwetu."

46 Nasi tunajua ya kwamba nyuma ya kila mkono asubuhi ya leo kulikuwa na shauku kubwa. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawajalia haja ya mioyo yao. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya mahali hapa, kanisa hili, sehemu hii ya Mwili wa Bwana Yesu, kwa wote. . .kwa ajili ya mchungaji wake, kwa ajili ya mashemasi wake, wadhamini, na washiriki wote wanaokuja hapa, kwa ajili ya watu wote waliokusanyika chini ya paa lake asubuhi ya leo, jengo hili; ninaomba ya kwamba utawabariki kwa wingi sana. Na iwe nyumba ya maombi, kama Yesu alivyosema, "Imeandikwa, nyumba ya Baba Yangu itaitwa nyumba ya sala."

47 Jalia kutoka hapa waende wahudumu sehemu zote za ulimwengu. Jalia matone ya umande wa rehema yawe halisi sana hapa mpaka nyukiasali wanaotafuta Chakula waje hapa kutoka sehemu zote za mjini wapate raha kwa ajili ya nafsi zao, Chakula kwa ajili ya nafsi zao. Tujalie, Bwana.

48 Sasa, tungeomba uyabariki maneno haya machache tutakayosoma, Bwana. Ninaomba ya kwamba utawatakasa wapande Mbegu katika mioyo ya watu, ipate kukua ikawa Miti mikubwa. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

49 Katika Warumi mlango wa 3, kifungu cha 3, ninasoma maneno haya:

> *Ni nini, basi, ikiwa baadhi yao hawakuamini? je, kutokuamini kwao kutaubatili uaminifu wa Mungu?*

50 Nitazungumza asubuhi ya leo, kwa dakika chache, juu ya *Kutokuamini Hakumzuii Mungu*. Huenda wengine wakafikiri kunamzuia, bali hakumzuii, Mungu anao utaratibu na mpango Wake, kama Yohana alivyosema, "Yeye anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Hiyo ni kweli. Mpango wake utaendelea vile vile tu.

51 Kutokuamini ni kwa kale kama Edeni, huko ndiko kulikozaliwa, ilikuwa huko Edeni. Nako kutokuamini ni kutilia shaka yale Mungu amesema. Sasa, mliona mahali kutokuamini kulikozaliwa kulikuwa na kiasi kikubwa cha Neno la Mungu kilichozingatiwa, kwa kuwa Shetani alimwambia Hawa, wakati aliposema, "Mungu amesema," yeye hakukana jambo hilo, ya kwamba Mungu amesema, "*hivi-na-vile*," bali alisema, "Hakika Mungu asingefanya jambo kama hilo." Mnaona, huko kulikuwa ni kuzaliwa kwa kutokuamini, kuondoa yodi moja kutoka kwa Neno kamilifu la Mungu. Hatuna budi kudumu moja kwa moja Nalo, haidhuru ni wapi, nini, ama vipi, maisha yetu na kadhalika hayana budi kulingana na BWANA ASEMA HIVI.

52 Na kama tukipata ufunuo wowote, ukiwasilishwa kwetu, ambao ni kinyume na Neno lililoandikwa, basi hatupaswi kamwe kuupokea, kwa sababu hivyo ndivyo hasa Shetani alivyomfanyia Hawa. Alikuwa na Neno, bali alikuwa akitafuta

Nuru mpya, naye Shetani akahakikisha kwamba ameipata. Kwa hiyo hatutaki kamwe kuongeza chochote kwenye Neno, wala kuondoa chochote kutoka kwenye Neno, bali tuliache tu jinsi lilivyo. Dumu moja kwa moja na Neno, kwa maana chochote kinyume ni kutokuamini.

53 Sasa, tunajua hilo katika siku hizi za mwisho na kulitazamia, imekuwa, sisi ndugu, wahudumu ambao tunaninii, tunajaribu kuishi karibu sana na Mungu tuwezavyo, kwa sababu tuna wajibu mtakatifu wa kulichunga kundi la Mungu, ambalo Roho Mtakatifu ametufanya waangalizi. Tunaliangalia hilo kundi kuliweka katika utaratibu, kuwalisha Chakula cha kondoo, nao kondoo hula kutoka kwenye Biblia, wana-kondoo wa Mungu, Yesu alisema, “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu,” moja kwa moja kwenye Neno.

54 Naye Paulo alisema katika Wagalatia 1:8, “Kama Malaika akiwaletea Injili nyingine yoyote isipokuwa ile ambayo mmepewa tayari, basi na alaaniwe.” Mnaona? Jinsi amri hiyo ilivyo imara, ya kwamba hatuna budi kudumu moja kwa moja na Neno, tusiliondokee. Mnaona? Naye Hawa akasogea tu kama *kivuli*, “Huenda ikawa labda, Mungu angepuuza tu hilo.”

55 Tunasikia mengi sana siku hizi kuhusu Mungu kuwa ni Mungu mwema, na hiyo ni kweli, Yeye ni Mungu mwema, tunaamini hilo, lakini Yeye pia ni Mungu wa hukumu. Ili awe mwema hana budi kuleta hukumu. Kuishika sheria Yake lazima kuwe—lazima kuwe na adhabu kwa sheria, la sivyo sheria haina nguvu. Kama kuna she—sheria inayosema ku—kupita taa ya kusimamisha ni kukiuka sheria, basi kama hakuna adhabu kwa sheria hiyo kutekelezwa, basi hiyo sheria haifai kitu hata kidogo, afadhali uipite tu ama chochote unachotaka, maana hakuna sheria.

56 Lakini unapovunja Neno hilo la Mungu kwa kanuni fulani ya imani ama mapokeo, umevuka mstari huo kati ya rehema na hukumu. Sawa. Huna budi kudumu moja kwa moja katika Neno, napenda hilo, moja kwa moja pamoja na Neno. “Hakuna nukta moja itakayoninii, wala yodi moja itakayopita. Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa.” Halina budi kuwa.

57 Jinsi ambavyo tungeweza kuchukua saa kadhaa hapa kurudi na kuweka msingi jinsi ambavyo, kama tungalikuwa na wakati, jinsi ambavyo sayansi, miaka mingi iliyopita, imejaribu kuyadhihaki mawazo yenyewe ya Mungu, wakijipatia wenyewe jina kuu, mafanikio fulani ambayo wangeweza kufanya wenyewe. Lakini mara wanapochimba na kujaribu kulikanusha Neno, Mungu hugeuka moja kwa moja na kuwaacha wachimbue kitu fulani kulithibitisha Hilo.

58 Kwa hiyo miaka michache iliyopita wakati kanisa la Kipentekoste lilipozaliwa, wa—walisema, “Ni kundi la ulokole,

ha—halitasimama kamwe," bila kujua kwamba huo ulikuwa ni mwenendo wa Mungu. Ilibidi Mungu kufanya hivyo, huo ndio wakati wake, ni wakati wake.

59 Kama nilivyosema mahali fulani si muda mrefu uliopita katika mmojawapo wa hiyo mikutano, labda hapa, ya kwamba Yohana alikuwa na hakika sana huyo alikuwa ndiye Yesu, hata kabla hajaona ishara ya Masihi, yule hua, Mungu akishuka kutoka Mbinguni katika mfano wa hua, Roho Mtakatifu akitoka Mbinguni, Sauti ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa," hicho ndicho alichopaswa kuona, Baba alimwambia hayo huko nyikani, "Yule ambaye utamwona Roho. . . " Lakini Yohana alikuwa na hakika *sana*.

Walimwuliza, kasema, "Je, wewe si yule Masihi? Si—si—si wewe ndiye, yule Nabii aliyekuwa aje? Je, wewe si *hiki* na *kile*?"

60 Akasema, "Mimi siye." Lakini kasema, "Kuna Mtu anayesimama miongoni mwenu sasa." Mnaona, alijua wakati ulikuwa umekaribia sana hata. . .Huyo tayari alikuwa katikati ya watu, kwa sababu alikuwa amtambulishe, naye alijua ya kwamba alikuwepo.

61 Nami ninaamini ya kwamba hivyo ndivyo lile Kanisa kuu la Mungu aliye hai limefanya katika siku hizi za mwisho. Ni kuwaletea watu utambuzi wa Mungu aliye hai miongoni mwa Kanisa. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu ya kuinuliwa kwake. Nalo Kanisa hilo linapaswa kurudi, si kwenye kanuni ya imani, kama fundisho la sharti la Kirumi ama chochote kile, linapaswa kurudi kwenye Biblia, kurudi kwenye Neno. Haidhuru linasema nini, a—ambatana tu na Neno, sio kutumia mawazo yetu wenyewe, dumu na Neno, kwa sababu ni ahadi ya Mungu.

62 Sasa, kutokuamini ni kitu cha kale huko nyuma kabisa katika Edeni, na kwanza kulikuja kwa ujanja sana, karibu ukweli. Sasa, kama mtu fulani alisema, "Ndugu Branham alipanda kwenda kwa Church of God asubuhi ya leo." Ni kweli. "Akakutana na mchungaji." Naam. "Alikuwa amevaa suti nyeusi na tai." Naam, hiyo ni kweli. "Akaketi upande wa kulia wa mchungaji." Kweli. "Akaamka na kuzungumza." Naam. Na labda hayo yote ni kweli, kila sehemu yake. Halafu wangesema, "Kabla tu, wakati alipofika mlangoni, alipofika mlangoni pale, alikunywa kinywaji kutoka kwenye chupa." Sasa, huo hapo uongo, lakini mengine yote ni kweli *kabisa*, mnaona, hayo mengine ni kweli *kabisa*, hata kitu hicho kimoja kidogo kinazonga kitu hicho chote na kukifanya uongo.

63 Vema, hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo. Yeye hutushusha kwenye kila kitu, na kukionyesha vizuri sana, naye ataingia na kukubaliana na karibu Neno lote la Mungu, bali hatachukua Neno lote la Mungu, na hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Atasema, "Ninaamini ya kwamba kuna kitu kama kuzaliwa upya, lakini kile nafikiri ndicho, ni badiliko la nia."

64 Lakini si badiliko la nia, ni kiumbe kipya. Sio. . . Ka—kanisa halihitaji ku—kukarabatiwa, linahitaji wongofu, linahitaji kuwa kiumbe kipya. Na kutokuamini kutakusukuma upande mmoja. Wengi wao wanasema, "Vema, sasa, ninaamini ya kwamba. . . Kwetu tunamwamini Roho Mtakatifu, bali tunaamini ya kwamba tunapomwamini Mungu, tunampokea Roho Mtakatifu." Sasa, mnaona jinsi hilo lilivyo karibu?

65 Vipi kama wanafunzi, baada ya siku sita Mathayo a—angemwambia Andrea, "Unajua nini? Ninaamini tayari tumempokea. Hebu tumkubali kwa imani"? Mnaona? Lisingetukia kamwe. Mnaona? Njia pekee waliyojua jinsi atakavyokuwa atakapokuja, walikuwa na Maandiko kuthibitisha jinsi atakavyokuwa wakati atakapokuja. Hiyo ni kweli.

66 Yoeli alisema, "Itakuwa," Yoeli 2:28, "itakuwa, siku za mwisho nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu na binti zenu watatabiri. Juu ya wajakazi Wangu na mtumishi wa kike nitaimwaga Roho Yangu. Nami nitaonyesha ishara mbinguni na duniani," kadhalika.

67 Isaya 28:18 ilisema, "Na itakuwa katika siku hizi za mwisho, kwamba meza zitajaa matapiko," na kadhalika, alisema, bali Neno litakuja, "Amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo na pale kidogo. Na mshikilie sana yaliyo mema. Kwa kuwa kwa midomo ya watu wageni na kwa lugha zingine nitasema na watu hawa. Na hii ndiyo raha, huku ni kuadhimisha sabato ambayo mnapaswa kuingia. Kwa haya yote, wasingeelewa, wakaondoka, wakitikisa vichwa vyao," na kadhalika. Kwa hiyo mnaona, hao wanafunzi walifundishwa kwa Neno.

Nasi tunajua ya kwamba katika siku hizi za mwisho ya kwamba itahitaji hii—hii. . . Mimi. . . ? Mimi. . . Natumaini sifanyi lolote baya.

68 Katika siku za mwisho kitakachohitajika ili kuchukua msimamo ni Kanisa lililofunzwa Kimaandiko, lisimame mstarini, kwa kuwa kutakuwako na uigaji wa kimwili utakaoinuka, Biblia ilisema, "Kama vile Yambre na Yane walivyopingana na Musa, ndivyo watakavyofanya watu hawa walioharibika akili zao kwa mambo ya Kweli." Naye Yesu alikuwa ndiye Kweli, "Neno Lako ni Kweli," kwa sababu, "Hapo, mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Nalo Neno la Mungu lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, hukata hata kugawanya mfupa, na ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo."

69 Tunatambua ya kwamba tuko katika ile siku ambapo chochote kinaweza kuonekana halisi *sana*, lakini hata hivyo, kama kiko nje ya Maandiko, achana nacho. Haidhuru ni mhemuko wa namna gani, unapata matokeo gani kwake, kama

si Maandiko kaa mbali nacho. Dumu moja kwa moja na Neno. Naam.

70 "Vema," unasema, "hiyo ni. . .Unawafanya watu, kutokuamini." La, ninajaribu kuwaleta kwenye imani. "Imani chanzo chake ni kusikia." Kusikia kanuni ya imani? Hiyo inaweza kuwa katika Shajara ya Mwaka, lakini hiyo si Biblia. Mnaona? "Kusikia Neno la Mungu," hilo ndilo linaloleta imani, kusikia Neno la Mungu, hilo huleta imani.

71 Sasa, kuna yapata dakika kumi na mbili zaidi zilizosalia, mimi. . .Sasa, mimi—mimi ni mwenda pole kupita kiasi tena. Kutokuamini hakumwangamizi Mungu, hakuharibu mpango Wake, hakuharibu kazi Zake, kunamwangamiza tu asiyeamini, kutokuamini kunamwangamiza tu asiyeamini.

72 Mmoja aliniambia si muda mrefu uliopita, mchungaji, alisema, alikuwa mfuasi wa shirika fulani zuri, naye akasema, "Tunampa mtu yeyote dola elfu moja, pesa taslimu, anayeweza kutoa," kabla tu ya matangazo yangu, "anayeweza kutoa tiba moja kwa uponyaji wa Kiungu. Nasi tutalipa." Naye alijua nilikuwa nikija nyuma yake huko Jonesboro, Arkansas.

73 Basi nikaenda kwenye matangazo yangu, na mara baada ya hayo matangazo, nilienda nikamchukua tabibu wa mjini, kwa mtu aliyekuwa na kansa shingoni mwake, ndipo nilipokuwa nikimwombea ikaanguka kutoka shingoni mwake, na kubingirika sakafuni, magazeti yakaandika habari zake.

74 Kwa hiyo nikamwomba huyo daktari, daktari wake, ambaye alikuwa ni rafiki yake, nami nikasema, "Daktari," Nilikuwa nimezungumza naye mara nyingi, huu ulikuwa ni mkutano mwingine baada ya hayo kutukia, nikasema, "unakumbuka kisa hicho?"

Akasema, "Vizuri."

"Je, unaweza kuchangia chochote, sayansi yoyote ya tiba, ambayo ingefanya hivyo?"

Kasema, "La, Bwana, siwezi."

"Basi itabidi iwe ni kitu Fulani cha kimbinguni kufanya hivyo."

Akasema, "Kweli."

Nikasema, "Nitakulipa kwa ajili ya wakati wako." Nilitaka kuchukua dola elfu moja kwa ajili ya umishenari.

75 Lakini nilipofika kwenye chumba cha kusomea cha mchungaji, kamwe hakuniona, naye akasema. . .Nikasema, "Nilisikia matangazo yako kwamba mngetoa dola elfu moja kwa mtu yeyote ambaye angeweza kutoa thibitisho la uponyaji wa Kiungu."

"Naam."

76 Nikasema, "Mimi. . .Unaweza, naomba ukaniandikie hiyo cheki, tafadhali." Nikasema, "Huyu *hapa* mtu huyo, huyu *hapa* daktari wake." Ndipo kumbe hizo dola elfu moja zilikuwa mahali fulani huko Texas, na kitu kama hicho.

Akasema, "Hebu nikuone. . .Nitamleta msichana mdogo hapa ndani na uniache niukate mkono wake, na hebu nikuone ukiuponya, ndipo nitaamini."

Nikasema, "Unahitaji sana uponyaji wa akili." Naam, bwana. Bila shaka, mtu yeyote aukate mkono wa mtoto!

77 Huyo ni ibilisi yule yule wa kale, aliyesema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, mbona, hebu. . .tufanyie mwujiza hapa mbele zetu. Hebu—hebu—hebu tuone mawe *haya* yakigeuka kuwa mkate." Mnaona? "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, shuka msalabani, tu—tutakuamini."

78 Angeweza kufanya hivyo, lakini angekuwa akimsikiliza ibilisi, Yeye alisema, "Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe." Mnaona? Hiyo ni kweli. "Ninafanya yale anayoniambia nifanye."

79 Kwa hiyo mnaona, wakati ushawishi huu unapotokea na kujaribu kuwaambia *hili*, *lile*, na *linginelo*, na, usiamini hilo; Ni Neno la Mungu.

80 Mhudumu huyu akaniambia, kasema, "Sijali," nilipotoka barazani mwake, "ni vitu vingapi ungeweza kutoa, bado siamini."

81 Nikasema, "Bila shaka huamini, wewe ni asiyeamini. Haikutumiwa wasioamini, Bwana, ilitumwa tu kwa waaminio, hao tu ndio watakaowahi kuiona."

82 "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena," asiyeamini, "lakini ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari," mwisho wa wakati. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Kama Yeye yu hai, hivi hatafanyiza kitu kile kile? Hivi Uzima Wake hautatenda kama ulivyotenda, kama unaishi ndani yako?

83 Sasa, kunamwangamiza tu asiyeamini. Na kulifanya hivyo hasa katika siku za Nuhu. Nuhu alikuwa mhubiri wa haki aliyelisikia Neno la Bwana, akaitayarisha safina kwa ajili ya kuiokoa nyumba yake. Naye alifanya nini wakati akiitayarisha safina hii? Aliwahubiria wasioamini. Sasa, Nuhu alikuwa mpotovu mbaya sana kwa hao wasioamini, lakini jambo pekee kutokuamini kwao kulifanya ilikuwa ni kuleta hukumu duniani.

84 Na hukumu yenyewe iliyomwangamiza asiyeamini ilikuwa ndiyo njia pekee ya kumwokoa Nuhu. Maji yale yale ya hukumu yaliyomwangamiza asiyeamini yalikuwa ndiyo kitu kilichoifanya safina ya Nuhu kuelea. Amina. Mnaona? Kwa hiyo kunamwangamiza tu asiyeamini. Hakuna uhusiano wowote na Mungu, hakumzuii, Yeye anaendelea mbele vivyo hivyo. Naam, bwana.

85 Sasa, imani, imani ni dhihaka kwa kila mtu ila Mungu na yule aliye nayo. Sasa, si dhihaka kwa Mungu, kwa sababu Yeye ndiye Mwanzilishi wa imani, wala si dhihaka kwa mtu aliye na imani, kwa sababu yeye anamwamini Mungu, kwa hiyo si dhihaka kwake. Mungu ndiye Mwanzilishi wake, Yeye aliiumba, na mtu aliyeipokea kutoka kwa Mungu . . .

86 Bila shaka si—si dhihaka kwa Mungu, kwa sababu Yeye aliiumba, Yeye anajua ni kitu gani, naye mwaminio anayeipokea, si jambo la dhihaka kwake kwa sababu hiyo ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo asiyoweza kuona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kusikia, bali anajua yapo. Si dhihaka kwake kwa sababu ni kama tu imetendeka, haimbidi kuwa na wasiwasi hata kidogo juu yake, anajua Mungu alilisema, na Mungu alilinena, hilo latosha kwake.

87 Vema, kwa hiyo tunataka kuwa na imani, Mungu anatutaka tuwe na imani. Wala kutokuamini hakutaiharibu mipango Yake, haitafanya chochote kwake, Yeye ataendelea moja kwa moja vivyo hivyo. Ningetaka kuona mtu akichukua kutokuamini kwao na kulisimamisha jua. "Vema," unasema, "ninii yako . . . " Loo, naam, ilifanya hivyo, Yoshua alifanya hivyo. Imani itafanya hivyo, ila kutokuamini kwako hakutafika popote. Hiyo ni kweli.

88 La. Angalia wingu likitokea, ndipo uone kama *kutokuamini* kwako kwamba haitanyesha, angalia kama haitanyesha vivyo hivyo. "Vema," unasema, "ingefaa chochote?" Loo, naam, imani itafanya hivyo. Mnaona, kutokuamini hakufai kitu hata kidogo.

89 Una—unatawaliwa na vitu viwili, ama unaamini, au huamini. Sasa, hebu na tuchukue kutokuamini tuone kunachofanya. Kunasababisha wasiwasi, na kunasababisha dhuluma, wala hakuwezi kukusaidia hata kidogo, kutokuamini hakuna faida hata kidogo.

90 Kama wewe, tuseme, kama ulikuwa upigwe risasi asubuhi kwenye mapambazuko, hainge—haingekusaidia hata kidogo kuhofia hilo, hata kidogo, ingelifanya tu kuwa baya zaidi kwako. Kwa hiyo hu—huwezi kufanya hivyo, si vizuri kufanya hivyo.

91 "Vema," unasema, "imani inafanya nini?" Ni . . . "Neno la Mungu linafanya nini?" Linaumba imani. "Vema, imani ingeweza kufanya nini kama utapigwa risasi asubuhi?" Ingeweza kunikomboa, imefanya hivyo mara nyingi. Hakika. Mnaona? Hakuna faida katika kutokuamini, manufaa yote yaliyopo, ni katika imani, kuliamini Neno la Mungu, kumwamini Mungu katika Neno Lake.

92 Sasa, hapa wakati fulani uliopita, kabla hawajaipiga marufuku ile Sanamu ya Uhuru, zawadi ya Marekani kutoka Ufaransa, sasa imepigwa marufuku nasikia, kwamba huwezi kuipanda, nilikuwa na majaliwa ya kuingia humo wakati mmoja. Nami nikapanda hata kwenye mkono wa—wa hiyo sanamu, na halafu, huko nje tukatembea mahali padogo, mimi pamoja

na huyo kiongozi, na kulikuwa na di—dirisha, nami nilikuwa nikitazama upande wa pili na kuwazia juu ya binamu yangu wakati aliporudi nyumbani kutoka jeshini, huko nje huku ameshambuliwa sana na kupigwa risasi.

93 Lakini hiyo meli ilipokuwa ikija kuelekea ufukoni, alisema, "Billy, wao—wao—wao walifingirisha viti vya magurudumu na—na kuwapandisha juu wagonjwa walio kwenye machela, wakati tungeweza kuona mbali sana," katika Vita vya Kwanza vya Dunia. Hiyo ilikuwa kabla ya hayo majengo makubwa kuja New York yangali makubwa sana, nao wangeweza kuona ile Sanamu ya Uhuru ikiinuka kutoka majini. Alisema walianza kucheza, "Nchi yangu ni kwa ajili yako, nchi tamu ya uhuru." Maskini mashujaa wa kale, waliokatwakatwa, waliochubuliwa, wakapigwa risasi, walemavu, walipoiona hiyo sanamu ikiinuka majini namna *hiyo*, alisema walianguka tu chini, wakaanza kupiga mayowe. Kwa nini? Moja kwa moja nyuma ya hiyo, mama alingojea, mpenzi alingojea, mke alingojea, watoto wachanga walingojea.

94 Nikawaza, "Kama ingemfanya askari kujisikia hivyo, ni nini hakitatukia tutakapouona ule msalaba wa kale unaoparuza ukining'inia kule? Askari mstaafu akijikokota na kuingia kutokana na majeraha na michubuko ya uwanja wa vita!" Loo, ninataka kusimama kwenye sitaha ya ile Meli ya Kale ya Sayuni na kuinua mikono yangu na kusema, "Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu!" Ama, "Loo, jinsi ninavyompenda Yesu."

95 Nilikuwa nikiangalia nje kupitia dirisha hilo na kuwazia hilo, nami nikaona chini *hapa* kando kando palikuwa na kundi la maskini shomoro waliokufa, nao walionekana kana kwamba walikuwa wameuawa hivi punde tu, ndipo nikamwambia yule kiongozi, nikasema, "Hao shomoro, kwani mliwapa sumu?"

Akasema, "La, la, hatukuwapa sumu."

Nikasema, "Vema, kwa nini wamelala wamekufa karibu na dirisha hili hapa?"

Akasema, "Waligongesha bongo zao dirishani."

Nami nikasema, "Hilo lilitokeaje?"

96 Akasema, "Hivi majuzi usiku kulikuwa na dhoruba." Kisha kasema, "Dhoruba ilipokuwa ikivuma, na pepo zikivuma, na miti ikitikisika, na radi ikimulika," akasema, "maskini ndege hao, wakijaribu kupata kimbilio," kasema, "waliingia kwenye mwangaza wa mnara huu," kisha kasema basi, "na kama wangaliutumia tu huo mwangaza kutafuta usalama, wangekuwa salama, lakini walichojaribu kufanya ni kuruka juu na kuipigapiga hiyo taa izime, nayo ikawapofusha tu, nao wakagongesha bongo zao zikatoka, basi wamelala mauti."

97 Kamwe sikusema lolote papo hapo, bali niliwazia, "Ni kweli jinsi gani! Wasioamini, badala ya kujaribu kuzima

Nuru ya ule Mnara," Neno la Mungu ndilo Nuru, "wakijaribu kuchukua Mnara huo na kwenda salama nao kwa Kristo, wanagongesha bongo zao zinatoka, wanakufa katika dhambi na aibu wakijaribu kuizima ile Nuru, wakati isingewezekana kabisa." Hakuwezi kuinuka makafiri wa kutosha, pepo wa kutosha kutoka kuzimu kuweza kuizima Nuru hiyo ya ulimwengu. "Mimi ndimi Nuru ya ulimwengu." Hawataizima kamwe.

98 Kwa hiyo kuna jambo moja tu la kufanya, inapoangaza kwenye njia yako, ifuate. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama. Mkikaa ndani Yangu," katika huo Mnara, "Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi mwaweza kuomba mtakalo, nanyi mtatendewa."

99 Mara nyingi nimehesabiwa. . . Sasa, ninaninii tu, nasema tu kama vile ningesema maskanini mwangu, nisingejisikia nyumbani zaidi huko, maskanini. "Ndugu Branham, mambo haya yanatendekaje? Ni kitu gani kinachotukia kwa *hili*, na *hili* linatukiaje?" Ni kukaa tu ndani ya Yesu, kuamini Neno Lake. Aliahidi kufanya hivyo, Naye atafanya hivyo.

100 Sasa, sina budi kuharakisha. Vema. Yesu alikuja ulimwenguni. . . Yapata tu tamshi moja zaidi. Nina yapata Maandiko hamsini yaliyoandikwa hapa juu ya hili, kwa hiyo, bali ni—nina Maandiko fulani tu, nami ninaweza kuangalia hapa chini na kuyarejea.

101 Sasa, Yesu, wakati alipokuja ulimwenguni, alikuja katika wakati wa kutokuamini kwingi mno. Hiyo ni kweli. Alikuja kwa njia ambayo ilimfanya asiyeamini kutokuamini zaidi. Mungu huvuta tu ninii. . . Yeye ni Baba wa ajabu sana. Alimleta moja kwa moja katika wakati ufaao, na kumpa ninii, jinsi watu walivyodhani, mtoto haramu, wala hawakumpeleka kwenye shule zozote, na kadhalika. Naye alikuwa ni Mvulana wa kipekee, lakini hata hivyo kulikuwa na kitu fulani kumhusu ambacho kilionekana kwamba yale aliyosema yalikuwa ni Kweli, yale aliyosema, yalitimia.

102 Wala kamwe hakujitwalia Mwenyewe sifa, bali alijiunganisha Mwenyewe na Mungu, "Si Mimi nizitendaye hizo kazi," Yeye alisema. "Mnadai Mungu kuwa ni Baba yenu, nanyi mnasema ndivyo alivyo, halafu hamniamini Mimi? Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo, hizo ndizo hati Zangu za utambulisho, ndizo zinazonishuhudia Mimi. Hizo ndizo zinazonena kama ni kweli ama si kweli. Someni Maandiko, yale Masihi aliyopaswa kufanya, yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Kwa hiyo Yeye alikuwa Neno la Mungu lililo hai, "Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi," Maandiko.

103 Kutokuamini kamwe hakukumkomesha, Yeye aliendelea tu kusonga mbele. Aliwaponya wagonjwa, akawafufua wafu, akawatakasa wenye ukoma, akaendelea mbele moja kwa moja, na wakati hawakuamini kwamba mambo kama hayo yangeweza kutukia, wala kutokuamini kwao hakukumzuia Yesu hata kidogo, aliendelea tu kufanya yale aliyopaswa kufanya, kamwe halikumsumbua hata kidogo.

104 Sasa, hapana budi kuwe na wasioamini, Mungu alitabiri hilo. Na kutakuwako na wasioamini kumi kwa mwaminio mmoja, zaidi ya hao, labda elfu moja kwa mmoja, kwa sababu Kanisa liko katika uchache, "Msiogope, enyi kundi *dogo*; ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa ninyi Ufalme." Kwa hiyo msitarajie kitu fulani kikubwa *mno*, ibilisi daima anatafuta kitu *kikubwa*, bali Mungu hujifanya Mwenyewe mdogo. Mungu, Mtoto mchanga katika hori, Yehova akilia. Ungeweza kuwazia? Yehova akicheza kama Mvulana tineja. Yeye alikuwa Mungu, Mungu alikuwa ndani Yake. Hiyo ni kweli. Alikuja kumdhihirisha Mungu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.

105 Kwa hiyo hebu angalia tu ninii, kile Kayafa angaliweza kukusanya, kile kilichoitisha kampeni kubwa. Wakati mwingine wachungaji kama huyu, wa kanisa lenye ukubwa wa kawaida, wakati mwingine labda huenda wakapata wazo kwamba "Kwa sababu mimi siko huko nje kama Billy Graham, ama Oral Roberts, ama kitu kama hicho, labda Mungu hanipendi vivyo hivyo." Sikiliza, kamwe usiamini hilo.

106 Baadhi ya mikutano yenye nguvu sana niliyopata kuwa nayo ilikuwa katika makanisa madogo sana, wakati mwingine watu saba au wanane nyumbani mahali fulani, tukiomba. Mnaona, Mungu aliahidi kukusanyika, haidhuru kanisa lilikuwa dogo jinsi gani, Yeye aliahidi kukusanyika pamoja nasi, "Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao."

107 Vema, kwa kumalizia, ninasema hivi: Kutokuamini hakumkomeshi Mungu, hakusimamishi mpango Wake, hakuusimamishi mwenendo Wake, hakusimamishi chochote ila asiyeamini. Humsimamisha katika dhambi yake, naye huyo hapo, amesimama akijiangalia.

108 Siku hizi wanasema hakuna kitu kama Roho Mtakatifu, bali hilo halimzuii, watu wanaendelea moja kwa moja kumpokea vivyo hivyo. Wanasema hakuna uponyaji wa Kiungu, bali wanaendelea moja kwa moja wakiponywa vile vile tu. Wanasema hakuna furaha, watu wanaendelea moja kwa moja kupaza sauti vile vile tu.

109 "Hakuna kitu kama ubatizo huu wa Roho Mtakatifu ambao ninyi Wapentekoste mnazungumzia." Lakini watu wanajazwa Naye kila siku. Huenda wasiweze kuuelezea, bali wanajua

wanao, hilo ndilo jambo muhimu. Kwa hiyo kutokuamini hakumzuii Mungu, tunajua tunaye, nina furaha sana kujihusisha na watu walio Naye.

Na tuombe. Mnampenda? Inua mkono wako.

110 Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana asubuhi ya leo kujua ya kwamba hakuna njia ya kumwelezea Mungu. Hatuwezi kumshusha Mungu kisayansi. Musa asingaliweza kuyachuma yale majani kutoka kwenye mti kuyapeleka kwenye maabara apate kujua ni dawa ya aina gani iliyokuwa imewekwa kwenye majani hayo, hata hayakuteketea, hakujaribu kufanya hivyo, aliketi tu chini na kuzungumza Nayo.

111 Ee Mungu, jalia kwamba watu hawa maskini, wanyenyekevu, walioko Phoenix, wakitangatanga huku na huko kwenye mitaa hii, ama, wakitembea polepole, hasa, huku na huko kwenye mitaa hii, inaonekana hawana mahali pa kwenda, hawana la kufanya, jalia waisikie Sauti ya Mungu kutoka kwenye maskani hii, na wengine mjini, na kuona Moto wa Mungu juu ya watu, kuwaona watu, jinsi wanavyotenda baada ya kumpokea, maisha yao ni kichaka kinachowaka moto.

112 Jalia wasijaribu kuona kisayansi kwamba yote yanahusu nini, lakini jalia waingie tu kwenye hili kanisa dogo na kuketi chini, wazungumze Naye. Nina hakika wataona, kama Musa, kwamba Yeye alisema, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO." MIMI NIKO kamwe hakuanza wala hana mwisho, Yeye alikuwako daima na atakuwako daima.

113 Tunakuamini Wewe, Mungu, nasi tunaomba ya kwamba utazidisha imani yetu, kwamba rehema kuu ya Mungu itaendelea kuwa pamoja nasi. Wabariki watu hawa humu ndani asubuhi ya leo, na kumtakasa mwa—mwaminio katika kiwango ambacho nguvu zote kuu za Mungu zinaweza kuachiliwa maishani mwao, hata watakuwa ni nyaraka zilizo hai, zinazosomwa na watu wote, nalo Neno la Mungu linaweza kuishi mioyoni na maishani mwao. Mbariki ndugu yetu mwenye rehema na mpendwa hapa, mchungaji, ninaomba, Mungu, ya kwamba utampa shauku ya moyo wake, kwake na kwa wapendwa wake, na kwa kanisa lake. Tujalie, Bwana.

114 Utusamehe kupungukiwa kwetu na uziweke nafsi zetu tayari kwa ajili ya kujazwa kwa Roho kunakokuja, kwa kuwa tunaamini ya kwamba huko kunakuja hivi karibuni, maana adui ameanza kuja kama mafuriko, nao walisema wangeinua ninii. . .Roho wa Mungu angeinua beramu dhidi yake. Tunatarajia katika siku hizi za mwisho, kama tulivyotaja, wakati mwanamwali aliyelala atakapoanza kulilia Mafuta, ndipo tunajua wakati umekaribia. Kwa hiyo, Bwana, tunafanya hesabu sasa hivi: Je, sisi ni waaminio? Tunaamini Neno lote? Zijaze taa zetu sana hata tutatoa Nuru gizani.

115 Bariki kusanyiko alasiri ya leo kwenye mkutano wa Ushirika wa Wafanyabiashara, ninaomba, Mungu, ya kwamba utawaokoa watu wengi alasiri ya leo. Pia, Baba Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utarudi kwenye kanisa hili dogo, hapa usiku wa leo, pamoja na hawa watu, na mahali pengine kote mjini ambapo watu wanakutanika. Tujalie, Baba.

116 Na siku moja tunatumaini ya kwamba tutafanya hivyo, wakati maneno haya ambayo yamesemwa asubuhi ya leo, na kanda hii ichezwe huko ng'ambo, mahali fulani katika anga kubwa za Mungu, kwamba sote tutakuwa kule bila waa wala kunyanzi, katika kutumainia ustahilifu wa Yesu pekee. Tujalie. Katika Jina Lake, tunaomba. Amina.

117 Mungu awabariki. Mnampenda? Ningetaka mnifanyie jambo fulani kabla tu sijamrudishia mchungaji ibada, ninajua ni saa sita, na ni wakati wetu wa kuondoka, yeye, nafikiri ana jambo lingine alilotaka kufanya, ama kusema, lakini kabla tu sijaondoka kwenda kujitayarisha kwa ajili ya mkutano huu mwingine unaokuja, ningetaka ninyi, mnipe fadhili.

118 Maskini kwaya hii, sasa ninataka kukupongeza, Bwana, juu ya kwaya inayoonekana nzuri, safi, iliyooshwa. Huenda mkafikiri nina kichaa, lakini kama ninacho, ningali niko sawa katika Neno. Hebu na tuimbe kwa mioyo yetu yote, *Nampenda*. Yule dada mpiga kinanda, waweza kwenda, uende pale? "Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza." Ninaupenda tu huo, nanyi je?

119 Loo, mimi ni Mkentaki. Kuna Wakentaki wowote hapa? Vema, nawatakia heri. Hmm! Si ajabu Arizona inaendelea vizuri sana. Loo, ajabu! Ndugu Ed Hooper, nilifikiri niliona, loo, uko mbali kidogo tu na Kentucky, nilikuwa nikimwazia kuwa Mkentaki pia, lakini ninaamini unatoka huko karibu na Carolina, mahali fulani huko juu, vizuri sana ninavyokumbuka.

120 Vema, kila mtu, kutoka kwenye vilindi vya moyo wako sasa, sote pamoja sasa, jinsi tunavyouimba kwenye tawi, mwajua, kwenye mikondo ya kijito, sasa kila mtu, kila mtu sasa.

> Nampenda . . . (Loo, jinsi hilo linavyosikika tamu!)
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

121 Huo ni mzuri? Mwajua, nilikuwa na maskini mhubiri aliyekuja kuniona. Mimi . . . Angehubiri kidogo, kisha arudi mbio na kunisalimia kwa mkono, aseme, "Utukufu kwa Mungu," kisha arudi mbio, ahubiri kidogo tena, maskini Ndugu Ryan. Nami nilikuwa nikiwazia . . . Siku moja nikasema, "Ndugu Ryan, ninataka kukuuliza jambo fulani. Mbona, kwa nini unarudi mbio na kunipa mikono wakati wote?"

122 Kasema, "Be—betri yangu hupungua moto, ninahitaji kuichaji kidogo," akasema. Kwa hiyo hii inanichaji kwa ajili ya alasiri ya leo, mnaona. Hebu tuuimbe huku tumeinua mikono yetu:

> Nampenda, na-. . .(Hilo ni zuri.)
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu (Vema, Ndugu, Mchungaji.)
> Mtini Kalvari.

123 Ni wangapi wanaopenda kupeana mikono? Mnapenda hilo? Loo, mimi, mwajua, nilikuwa Mbaptisti, bali kwa namna fulani nilikuwa Mbaptisti anayepeana mikono, lakini huko kamwe siko kulikotoka; ninapenda kupeana mikono vizuri.

124 Wakati fulani uliopita, mke wangu hayuko pamoja nami asubuhi ya leo, na Dada Sothmann, mwajua, kamwe msimwambie, mnaona, nilishuka kwenda katikati ya mji pamoja naye. Ninapenda kupeana mikono huku kuzuri kwa mtindo wa kale, mwajua. Ni—nikaenda katikati ya mji, ndi—ndipo mama fulani akasema, "Halo, Dada Branham."

Nami sikumsikia akisema chochote, nikasema, "Mpenzi, huyo—huyo—huyo mama alizungumza nawe."

Akasema, "Nilizungumza naye."

"Vema," nikasema, "nina hakika hakusikia, mimi sikuisikia, niko karibu *hivi* nawe."

Akasema, "Loo, nilitabasamu."

Nikasema, "Sasa, maskini tabasamu dogo la kipumbavu!" Na—na—napenda—napenda kupeana mikono halisi, nanyi je? Je, hampendi hilo?

125 Wakati fulani uliopita, huko chini kabisa, uh, hili ni baya sana, Mchungaji, samahani, huko chini kabisa, nilikuwa, nilienda huko chini Florida. Tulikuwa na mkutano, nasi tulikuwa na hema kubwa huko nje yapata, loo, maelfu mengi ya watu walikuwa wamekusanyika kwa ajili ya uponyaji, na, mwajua, ibada za uponyaji, mnajua jinsi zilivyo, kuvutana na kupinda, basi mmoja wa hao ndugu akanijia, kasema, "Mwinyi mwanamke anataka kukuona."

Nikasema, "Ati *nani*?" Sikujua huyo ndugu alikuwa akizungumzia nini.

Kasema, "Mwinyi mwanamke."

126 Nikasema, "*Mwinyi* mwanamke ni nini?" Nilifikiri huenda ikawa ni Mholanzi, kama wanavyoita Mholanzi Aliyepotea hapa juu, mahali fulani. Huenda alikuwa ni Mholanzi aliyepotea pia, mwajua. Kwa hiyo nikasema, "Sielewi."

Akasema, "Mbona, ni—ni mwanamke anayemiliki mali hii yote kupitia hapa."

Nami nikasema, "Vema, angalia, kuna yapata wagonjwa elfu tano huko nje wanaojaribu kuingia, pia."

"Loo," akasema, "lakini huyu ni mwanamke Mwinyi, lazima umwone."

Nami, loo, nikasema, "Yeye si zaidi ya mtu mwingine yeyote, sivyo? Unaona, yeye ni mwanadamu tu."

Naye akasema, "Unapotoka kwenye hema hapa, atakuwepo."

127 Nami nikamwangalia. Alikuja (Sasa, mimi . . . tafadhali msifikiri huku ni kukufuru, natumaini halisikiki hivyo.), bali alikuwa na jozi ya miwani kwenye kijiti. Sasa, unajua hutaangalia kupitia kwenye kijiti namna *hiyo* na kuona chochote, alikuwa na miwani kwenye kijiti, namna *hii*.

Naye akasema, "*Hivi* wewe ni *Daktari* Branham?"

Nami nikasema, "La, Mama. La, la, la, la." Nikasema, "Mimi ni Ndugu Branham."

Akasema, "*Nimefurahi sana*."

128 Ndipo akaunyosha mkono huo huko nje ukiwa na dhahabu ya kutosha kuwatuma wamishenari dazani moja kote ulimwenguni mara kumi. Naye akainua mkono wake juu, namna *hii*. Sasa, hiyo si njia ya kupeana mkono, nikanyosha mkono nikaushika mkono huo mkubwa mnene na kuukamata, nikasema, "Ushushe hapa chini, nipate kukujua nitakapokuona tena."

129 Ninapenda kupeana mikono kuzuri, nanyi je? Hebu na tupeane huo mmoja kwa mwingine, tunapoimba *Nampenda* tena. Kila mtu sasa:

> Nampenda . . . (Mungu akubariki, Ndugu. Mungu akubariki, ndugu yangu.)
> . . . alinipenda kwanza (Hiyo ni kweli.)
> Na kununua wokovu wangu
> . . . Kalvari

130 Mpaka nitakapowaona tena, Mungu awabariki. Sasa hebu na tumwinulie mikono yetu.

> Nampenda . . . (Ndugu, Mchungaji . . . ? . . . )

62-0128M Kutokuamini Hakumzuii Mungu
Church Of God
Phoenix, Arizona Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org